Misri na Kenya

مصر - أفريقيا 2019

Egypt - Africa 2019

Mkuu wa Bodi ya Wakurugenzi

Diaa Rashwan

Mwandishi

Abdelmoeti Abouzaid

Mkuu wa Sekta ya Vyombo vya Habari za Nje

Kimefasiriwa na :
Asmaa El-Sayed Belal
Basant Khaled Shawki
Enas Ebrahim Ahmed
Laila Alaa-Eldeen

Kimerejewa na :
Issa Ramadhani Majilanga

Utoaji wa kisanaa:
M/ Rania Saleh

Jalada la Kitabu :
Abeer Ahmed

Msimamizi wa Uchapichaji
M/Iman gaafar

Usimamizi wa Kiufundi
Hossam Ameen

Kimechapishwa na

Mamlaka Kuu ya Habari

3, Barabara ya Al-Estad Al-Bahary-Mji wa Nasr -Kairo

Simu :002 02 22616716

Fax.: 002 02 22608444

Barua Pepe:
african_perspectives@yahoo.com
Site Internet :
africa.sis.gov.eg

KAIRO

2019

Toleo hili linasambazwa bure

na haliuzwi

Yaliyomo

Mfululizo Huu:.....5

Kitabu hiki :.....7

Sura ya kwanza: Maendeleo ya mahusiano kati ya Misri na Kenya.....9

Sura ya pili: Mahusiano ya Kisiasa 13

Sura ya tatu: Mahusiano ya kiuchumi na kibiashara.....27

Sura ya nne: Ushirikiano kuhusu Maji ya Mto wa Nile.....39

Sura ya tano: Mahusiano ya kiutamaduni na vyombo vya habari.....43

Mfululizo huu:

Uenyekiti wa Misri kwa Umoja wa Afrika kwa mwaka wa 2019 ni kama kuthamini undugu wa nchi za Afrika, na kuiamini Misri na Rais wake, Rais Abdel Fattah Al-Sisi.

Nchi ya Misri, katika ngazi zote, inafanya kazi hii kama heshima, jukumu na wajibu wa kutimiza ili kuhakikisha manufaa kwa bara la ww na kukuza ushirikiano kati ya raia wake.

Mamlaka kuu ya habari ilianzisha mfululizo wa shughuli katika nyanja za vyombo vya habari mubashara (moja kwa moja) kielektroniki na kuchapishwa, na hayo ilikuja kama sehemu ya jukumu lake kama taasisi ya habari ya umma ya kimisri.

Miongoni mwa shughuli hizi ni mfululizo wa vitabu ambavyo vinachapishwa katika karatasi na kwenye tovuti za Mamlaka kuu ya habari.

Mfululizo huo ulianza na kitabu kinachoitwa «Misri katika Afrika», kilichofuatiwa na vitabu kadhaa, kila kitabu kinazungumzia nchi za Afrika na uhusiano wake na Misri, ili kukuza ushirikiano kati ya raia wa Afrika, kuimarisha ujuzi wa raia wa Misri kuhusu ndugu zao wa nchi za Afrika na kuzungumza na raia wa Afrika kwa lugha zao.

Kitabu hiki:

Mahusiano kati ya Misri na Kenya yameshuhudia maendeleo makubwa tangu mwaka 2014, hasa katika mfumo wa mawasiliano kati ya uongozi wa kisiasa wa nchi hizo mbili kwa uongozi wa Rais Abdul Fattah El-Sisi na Rais wa Kenya Uhuru Kenyatta.

Maendeleo hayo yanategemea misingi ya kijiografia na kihistoria na matarajio ya pamoja kwa faida ya raia wa nchi mbili na bara la Afrika kwa ujumla. Misiri na Kenya zimeunganishwa na mshipa mmoja (Mto wa Nile). Ushirikiano wa kisasa kati nchi mbili unategemea historia ndefu ya mapambano na ushirikiano wa pamoja ambao ulianza katika miaka ya sitini ya karne iliyopita chini ya utawala wa kiongozi Gamal Abdel Nasser wakati wa msaada wake kwa harakati za ukombozi wa Kenya zilizo kuwa zikiongozwa na Jomo Kenyatta.

Kitabu hiki, Misri na Kenya, ni miongoni mwa mfululizo wa vitabu «Misri na Afrika» ambavyo vinatolewa na Mamlaka Kuu ya Habari wakati wa tukio la uenyekiti wa Misri kwa Umoja wa Afrika 2019.

Kitabu hiki kinachangia kukuza mahusiano kati ya raia wa nchi mbili Misiri na Kenya. Pia kinajumuisha maelezo ya msingi kuhusu Jamhuri ya Kenya katika nyanja zote za kihistoria, kijiografia na kimakazi, pamoja na mfumo wa kisiasa, maendeleo ya kiuchumi, fursa za uwekezaji na ukuaji, vile vile viashiria muhimu katika nyanja hizo. Pamoja na utalii na vivutio maarufu zaidi nchini Kenya ili kukuza ujuzi wa raia wa Misiri na wasomaji kwa nchi ya Kenya na raia wake, na hayo yanategemea vyanzo vya kimisri na kikenya.

“Misri na Kenya zimeunganishwa na mshipa mmoja nayo ni Mto wa Nile, na historia ndefu ya ushirikiano na matarajio ya pamoja. Nchi hizo mbili zinafanya juhudi kubwa ili kuhakikisha maendeleo kwa raia wao kulingana na uwezo wao mkubwa na eneo lao la kimkakati. Na sisi tunaamini kwamba ushirikiano wa kiuchumi kati ya nchi mbili utakuwa sababu kuu katika kuhakikisha malengo haya . Leo nimeshuhudia majadiliano yetu ya kujadili njia za kukuza mahusiano ya kiuchumi na kibiashara kati ya nchi hizo mbili kwa njia ambayo inahakikisha masilahi ya pamoja na matarajio ya raia wetu ndugu.**”**

Rais Abdul Fattah El-Sisi wakati wa mkutano wake na Rais Uhuru Kenyatta Februari 18, 2017

“Kuna makubaliano kadhaa yanayohusu maswala mbali mbali kama kilimo, mifugo, utalii, biashara, elimu, utamaduni, uwekezaji na diplomasia. Huu ni uthibitisho juu ya ushirikiano wa kina na urafiki kati ya nchi zetu mbili, tunasonga mbele, tunachohitajika kufanya ni kurejea makubaliano haya na kuhakikisha utekelezaji wake kamili ili Tuweza kuanza kuona makubaliano haya yanageuzwa kwa mipango na miradi yenye faida ya pamoja kwa nchi zetu mbili.**”**

Rais Uhuru Kenyatta wakati wa mkutano wake na Rais El-Sisi Februari, 2017

Sura ya kwanza
Maendeleo ya mahusiano kati ya Misri na Jamhuri ya Kenya

Mahusiano kati ya Misri na Kenya yalianza kabla ya Kenya kupata uhuru wake ambapo wakati wa utawala wa Rais Gamal Abdel Nasser, Misri iliunga mkono harakati za «Mao mao» za Kenya kupitia kampeni ya vyombo vya habari na kidiplomasia dhidi ya ukoloni wa Uingereza kwa Kenya. Na Misri ilianzisha Kituo cha redio kwa jina la «Sauti ya Afrika» kilichotengwa kwa raia wa Kenya ili kuwaunga mkono katika mapambano yao kwa ajili ya kupata uhuru.na kituo cha redio hiki ni cha kwanza kwa lugha ya Kiswahili kutoka nchi za Afrika ili kuunga mkono Kenya kupata uhuru wake.

Misri ilifanya suala la «Mao mao» kuwa suala la Kiafrika na ilifanya juhudi kubwa ili kuachiliwa huru kiongozi wa Kenya Jomo Kenyatta, aliyefungwa gerezeni na ukoloni wa Uingereza katika mwaka wa 1961. Kairo ilikuwa mji Mkuu wa kwanza unawapokea na kuwasaidia wapiganaji wa Kenya wanaongozwa na Eugenja Odinga, Tom Mboya, James Jeshoro, Joseph Morupi na wengine kama wanachama wa chama cha Umoja wa Kitaifa wa Kiafrika wa Kenya (KANU) na Chama cha Umoja wa Kidemokrasia wa Kenya (KADU). Vyama hivyo viwili vilifungua ofisi huko Kairo katika kipindi hiki, na matokeo ya juhudi za kimisri katika kuunga mkono mapambano ya Kenya ili Kenya ipata uhuru wake na ilipata uhuru wake mwaka wa 1963.

Mnamo 1964, Kenya ikawa jamhuri na ilianza mahusiano ya kidiplomasia na Misiri na kufungua ubalozi wake Mkoani Kairo. Wakati wa kupitishwa kwa nyaraka za balozi wa kwanza wa Jamhuri ya Kenya huko Kairo, Rais Gamal Abd El-Nasser alionesha kufurahishwa kwake

kwa mapambano ya raia wa Kenya kwa ajili ya kupata uhuru kwa uongozi wa « Jomo Kenyatta» ambaye ni Rais wa kwanza kwa Kenya baada ya uhuru. Abdel Nasser alionesha kuwa tayari kwa ushirikiano na Kenya na nchi zote za Afrika ili kuimarisha nguvu ya Afrika na kukuza rasilimali zake, na hivyo kuchangia kuimarisha umoja wake

Katika mwaka wa1964, Misri ilikaribisha Mkutano wa Kilele cha Pili wa kiafrika. Pembezoni mwa vikao vya mkutano huo, Rais Nasser alionesha kuwa tayari kwa ushirikiano wa kijeshi na Kenya na Rais Kenyatta alimjibu kwa kuelezea nia yake ya kuwaondoa wanajeshi wa Uingereza katika nchi yake, kwa hivyo Misri iliunga mkono Kenya katika kujenga Jeshi la Kitaifa la Kenya.

Na katika muktadhaa huu Rais Jomo Kenyatta alisema «Tutamkumbusha Nasser kwamba misaada yake kwa Afrika imeokoa nchi nyingi za kiafrika».

Mnamo 1967, mradi wa «Hydromet» ulianzishwa kwa kushiriki Misiri na Kenya miongoni mwa nchi tano za Bonde la Mto wa Nile na baadaye nchi zingine nne zilijiunga kwa mradi huo. Mradi huo ulilenga kufanya utafiti wa hali ya hewa na maji kwa bonde la maziwa ya Tropiki, kuweka mipango ya maendeleo ya rasilimali ya maji na kufanya utafiti wa uwiano wa maji kwa Mto wa Nile.

Kenya ilikuwa miongoni mwa nchi zilizovunja mahusiano yake ya kidiplomasia na Israel baada ya vita vya Oktoba 1973, kiasi kwamba baraza la Mawaziri la shirikisho la nchi za Afrika lilofanyika katika mwezi wa Novemba 1973,walifanya uamuzi wa kuvunja mahusiano ya kidiplomasia na Israeal , na kuiomba kuondoka maeneo yaliyo chini ya uvamizi na kuwapa wananchi wa palestina haki ya kujiamulia mambo yake.

Katika mwezi wa Novemba mwaka wa 1984 , Rais wa zamani alifanya ziara nchini Kenya ikiwa ni miongoni mwa ziara za nchi za Afrika ,na kwamba alizuru Zaire ,Somalia na Tanzania ,aidha alionesha kwamba misri itakuwa daraja muhimu baina ya nchi za kiarabu na wananchi wa Afrika kama mpatanishi ili kutatua migogoro ya bara la Afrika.

Katika mwaka wa 1998 , Misri ilijiunga na mkataba wa COMESA ambao unajumuisha nchi za Afrika 22, Kenya ikiwa ni mojawapo ya nchi zilizo tia saini masharti ya mkataba wakati ulipofanyika mkutano wa Mawaziri katika mji mkuu wa Malawi mwaka wa 1995, COMESA kwa upande wa Misri inazingatia ni muhimu sana katika nyanja ya Kijiografia na kisiasa, kwa kuwa Misri ipo katika eneo bora la kijiografia na ipo karibu na ulimwengu wa kiarabu , eneo la pembe ya Afrika , na nchi za bonde la Mto Nile , ni kama mkanda unaoizunguka Misri.

Kukua mahusiano ya pande mbili

Misri imeendeleza ushirikiano wake na Kenya katika viwango vyote, na mahusiano ya urafiki wa kidugu kati ya nchi mbili ndugu Misri na Kenya undugu huu umetokea wakati wa shida, ni katika kupambana na majanga ya asili kama ukame na mafuriko, kwa kutoa vyakula , matibabu na misaada ya kiufundi kwa watu wa Kenya.

- Katika mfumo wa ushirikiano wa kimahakama na ushauriano kuhusu mifumo ya sheria, Jaji Mkuu wa Kenya, Johnson Evens Jibshiro, alitembelea Misri kutoka 1-3 Desemba 2008 ili kufahamu juu ya kazi ya Wizara ya Sheria ya Misri na mfumo wake wa kisheria na ilifanyika idadi kadhaa ya mikutano na wenzake katika Wizara ya Sheria ya Misiri.

  Mnamo tarehe 17-18 Juni 2009, Kenneth Marinde, Spika wa Bunge la Kenya, alitembelea Misri ili kuhudhuria kikao cha pili cha Kongamano la Bunge la Nchi za Bonde la Mto wa Nile.

- Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Kenya Kalonzo Masyuka aliongoza ujumbe kutoka nchi yake ili kushiriki katika shughuli za mkutano wa kilele wa nchi zisizopendelea upande wowote uliofanyika mjini Sharm El-Sheikh katikati ya Julai 2009, na alikutana na Waziri wa Mambo ya nje wa Misri na akielezea kuthamini kwake uhusiano wa ndani wa nchi mbili, na alisisitiza azimio la Kenya kusukuma mbele mahusiano yale, hasa kuhusu kukuza viwango vya ubadilishanaji wa biashara kati ya nchi hizo mbili.

Kupitia mkutano wa nne wa Mawaziri kwa ajili ya kusaidiana kati ya China na Afrika mkutano ambao ulioitishwa na Misri katika mji wa Sharmu Sheikh katika kipindi cha kuanzia 8-9 /11/2009, na mkutano huo ulihudhuriwa na Waziri wa Mambo ya nje wa Kenya Moses Witangola akiongozana na wajumbe kutoka katika mji wake, Witangola alikutana pembezoni mwa mkutano wa Mawaziri na Waziri wa Mambo ya nje wa Misri pale walipofanya mazungumzo kuhusiana na matukio mengi yenye umuhimu wa pamoja hasa kusaidiana katika nyanja ya kuendeleza vyanzo vya maji nchini Kenya, na uwezo wa Misri kuisaidia Kenya kwa ajili ya kukabiliana na kupungua kwa mvua na na kurejea kuiandaa misitu yenye mvuto wa mvua.

Na katika mwezi wa mei 2010 waziri mkuu wa Kenya Laila Odinga lifanya ziara ya kuelekea nchini Misri akasisitiza kupitia mkutano wake na wausika wa kimisri kwamba Kenya «haiwezekani ikafikiria au ikaelekea katika kuyadhuru masilahi ya Misri ya kimaji».

Katika April 2011 Naibu Waziri wa Mambo ya nje wa Kenya Rechard Unionka alifanya ziara ya Kairo kwa ajili ya kufanya mashauriano ya kisiasa pamoja na maofisa kadhaa nchini Misri.

sura ya pili:
Mahusiano ya kisiasa

Misri inafungamana na Kenya kupitia mshipa mmoja wa uhai nao ni Mto wa Nale, na historia ndefu inayotokana na kusaidiana katika ujenzi na zinashirikiana katika malengo na mielekeo, nchi mbili hizi zinafanya kazi ya kufikia maendeleo na utulivu wa kiuchumi kwa wananchi wake zikitegemea uwezo wake mkubwa na nafasi yake ya kimiundombinu iliyo ya kipekee, kwani Misri ipo katikati ya mabara matatu ya ulimwengu wa zamani na ikipakana na bahari mbili muhimu nazo ni bahari ya Shamu na bahari ya Meditereniani na huku ikipitiwa na mfereji wa Suez, ni mapitio muhimu ya bahari kwa kiwango cha kimataifa , na ina Ustaarabu wa kale na mahusiano mazuri na nchi zote za bara la Afrika, ama Kenya inajulikana kwa mipaka yake ya Mashariki inayopakana katika bahari ya Hindi ni jambo ambalo limeifanya kuwa ni mzunguko muhimu wa muunganiko wa kibiashara kati ya Mataifa ya Kiarabu na Mataifa ya bara la Afrika tokea karne nyingi, kama ilivyojiweka nafasi yake ya kijiografia ya kipekee kwa ajili ya kusimamia nafasi yake ya uongozi katika eneo la Afrika Mashariki na nje yake.

Mahusiano ya Misri na Kenya baada ya mwaka 2014

Mahusiano kati ya Misri na Kenya tokea mwaka 2014 yalishuhudia maendeleo mazuri na ukuaji wenye kuzingatiwa katika nyanja zote, hakika Misri ilipita njia mbili katika mahusiano yake na Kenya, njia ya kwanza ni mahusiano ya pade mbili na ziara za pande mbili ambazo zinalenga kusaidiana kati yao, ama njia ya pili inahusiana na kusaidiana katika sekta ya maji kwa kuzingatia kwamba ni nchi mbili muhimu miongoni mwa mjumuiko wa nchi za Bonde la Mto Nile.

Na katika mwaka 18/2/2017 Rais Abdulfattah Al-Sisi alifanya ziara rasmi nchini Kenya ziara ambayo ni ya kwanza ya aina yake kwa Rais wa Misri tokea miaka 33, na akakutana na Rais wa Kenya.Uhuru Kinyata, pale walipofanya kikao cha mazungumzo yanayohusu pande mbili kikifuatiwa na mkutano wa pamoja ukihudhuriwa na wajumbe wa nchi mbili, na Rais Kinyata alielezea furaha ya wananchi wa Kenya kwa kutembelewa na Rais Al-Sisi, akiashiria kwamba ziara hiyo imekuja kwa ajili ya kuyavisha taji mahusiao ya kipekee ambayo yanazifunga nchi mbili na mataifa mawili yaliyo ndugu, hali ya kuwa ni mwenye kujenga nafasi ya kihistoria ambayo inasimamiwa na Misri..Katika kuunga mkono harakati za kupigania uhuru katika mataifa mbali mbali ya kiafrika, huku akitilia msisitizo kwamba ziara hiyo inaashiria kutilia umuhimu Misri mahusiano yake na mataifa ya kiafrika, na akisisitiza kurudi kwake kwa mara nyingine katika nafasi yake ya asili ya uongozi katika bara.

Kwa upande wake, Rais Al-Sisi alisisitiza lengo la Misri katika kuuendeleza uhusiano wake na Kenya katika nyanja zote, na kufanya kazi pamoja kwa ajili ya kuhakikisha maslahi ya nchi mbili yanapatikana, na Rais Al-Sisi alitoa mualiko rasmi kwa Rais wa Kenya kuitembelea Misri kwa ajili ya kuuendeleza ushauriano na ushirikiano kati ya pande mbili.

Pande hizo mbili zilijadiliana njia za kuongeza mahusiano ya kiuchumi kati ya nchi mbili, Marais hao wawili walisisitiza umuhimu wa kuzidi kusaidiana hasa kupitia uwanachama wa nchi mbili katika soko la pamoja la Mashariki na kusini mwa Afrika (COMESA), na katika mfumo huu, Marais wawili walijadili njia za kuongeza kubadilishana biashara, pia walijadili matokeo ya mkutano wa kwanza wa Balaza la Biashara la Misri na Kenya ambalo lilifanyika Nairobi, na yakatimia kupitia mkutano huo makubaliano ya kuongeza kubadilishana biashara kufikia dola bilioni moja kwa muda wa miaka miwili kupitia miradi kadhaa ya pamoja katika nyanja mbalimbali.

Marais hao wawili walikubaliana kufanya mikutano ya kikao cha saba cha kamati ya pamoja chini ya uenyekiti wa mawaziri wawili wa mambo ya nje mwaka 2017, pamoja na maandalizi mazuri ili kusababisha kuunga mkono na maendeleo ya mahusiano kati ya nchi

hizo mbili katika nyanja mbali mbali. Marais hao wawili pia walisisitiza umuhimu wa kuamsha mikataba iliyosainiwa hapo awali kati ya pande hizo mbili, na kufanya mikataba mipya, hasa katika uwanja wa kuzuia ushuru mara mbili na kulinda uwekezaji, kwa lengo la kutoa hali ya hewa inayofaa ili kuongeza ushirikiano katika nyanja za uchumi na uwekezaji, na Rais Kenyatta alisifu misaada ya kiufundi iliyotolewa na Misri ili kusaidia na kujenga uwezo wa Wakenya katika nyanja mbali mbali, pamoja na mchango wake mzuri Katika miradi kadhaa ya maendeleo katika nyanja za afya, kilimo na umwagiliaji.

Katika suala hili, Rais Al-Sisi alisisitiza hamu ya Misri ya kuendelea kutoa msaada wa kiufundi ili kujenga uwezo na mafunzo nchini Kenya, akikaribisha ombi la upande wa Kenya; Misiri inatoa vifaa vya matibabu na madaktari katika hospitali ya kijeshi inayojengwa hivi sasa katika mji mkuu wa Nairobi, ambapo Rais aliamua kutuma ujumbe wa wataalamu ili kutembelea hospitali na kufahamu mahitaji yake haraka iwezekanavyo.

Mazungumzo hayo pia yaligusia maswala mbali mbali ya kikanda yenye masilahi ya pamoja, hasa kuhusu maendeleo ya hali nchini kusini mwa Sudan na Somalia. Marais hao wawili walisisitiza hitaji la kuendelea uratibu kati yao ili kufanya kazi kwa lengo la kufikia amani na utulivu katika eneo hilo. Rais al-Sisi alisisitiza kwamba Misri iko tayari kwa kuendelea mashauriano pamoja na upande wa Kenya ili kuimarisha utulivu na kufanikisha amani na usalama barani Afrika kwa ujumla, na uratibu katika maswala tofauti ya kikanda na ya kimataifa.

Marais wawili pia walijadili maswala kadhaa ya Umoja wa Mataifa «UN» , ambapo waliafikiana kimaoni na kukubaliana kuendelea na taratibu za mchakato wa marekebisho ya shirika la kimataifa .. Rais wa Kenya pia aliomba msaada wa Misri katika kuendelea kukaribisha Nairobi Makao Makuu ya Mashirika kadhaa ya kimataifa ya Umoja wa Mataifa.

Mwishoni mwa ziara yake Nairobi, Rais Al-Sisi alifanya ziara kwa Kituo cha Umoja wa Mataifa barani Afrika, ambapo alisikiliza maelezo ya sehemu muhimu zaidi za Kituo hicho, ambacho kinajumuisha Makao Makuu kadhaa ya mashirika ya kimataifa kama vile Programu

ya Mazingira ya Umoja wa Mataifa UN (UNEP) na Programu ya Umoja wa Makazi ya Wananchi (Habitat),pamoja na makao ya kikanda kwa mashirika kadhaa kama vile Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) na Shirika la Kazi la Kimataifa (ILO).

Mashauriano kwa njia ya simu kati ya Marais wawili

Rais Abdul-Fattah Al-Sisi alimpigia simu Rais wa Kenya Uhuru Kinyata Novemba 24, 2018 ambapo walijadili maswala kadhaa yenye shughuli za pamoja za bara la Afrika, hasa baada ya maendeleo ya kisiasa katika Pembe yaAfrika ambapo imesisitiza kuunga mkono juhudi za amani huko Sudani Kusini,pamoja na kuunga mkono juhudi za kufikia utulivu nchini somali.

Marais wawili walikubaliana kuongeza uratibu wa pamoja katika kipindi kijacho ili kuimarisha mahusiano ya ushirikiano wa pamoja hasa katika uwanja wa kubadilishana biashara na uwekezaji, pamoja na kuongeza njia za mashauriano na kubadilishana maoni kuhusu maswala muhimu zaidi ya sasa katika kanda hasa baada ya Uenyekiti wa Misri mwaka 2019 .Pia Rais Al-Sisi alitoa wito mpya kwa mwenzake wa Kenya ili kuzuru Misri karibuni ili kuunga mahusiano mema ya undugu kati ya nchi marafiki.

Agosti 15, 2017 Rais Abdel Fattah Al-Sisi alimpigia simu Rais wa Kenya Uhuru kenyatta ili kumpongeza kwa kuchaguliwa tena kuwa Rais wa Kenya akielezea matumani yake ya kweli ya mafanikio kwa Rais wa Kenya na maendeleo na ustawi kwa Kenya.

Rais Al-Sis alielezea wakati wa mazungumzo yake kwa njia ya simu, kuthamini kwake mahusiano ya pamoja kati ya Misri na Kenya, akisisitiza nia ya Misri ya kuendelea kusukuma mahusiano hayo na kuyaendeleza katika nyanja zote za Ushirikiano kati ya nchi mbili.

Kwa upande wake; Rais wa Kenya alielezea shukrani zake za dhati kwa Rais kwa kumpongeza kwa dhati akisifu mahusiano thabiti yanayojumuisha nchi mbili, akielezea nia ya nchi yake kuimarisha mahusiano yake na Misri katika nyanja zote na kuyasukuma mbele

kufikia upeo mpana. pia Marais Mawili walikubaliana kuendelea kuwasiliana kuratibu na mashauriano ya kina juu ya ngazi za nchi mbili na kikanda ili kupambana na changamoto zinazokabili bara la Afrika.

Mahusiano ya pamoja

Tarehe 3/3/2019 Rais Abdelfattah Al-Sisi alimpokea Monika Juma, Waziri wa mambo ya nje ya kenya na ujumbe aliofuatana nao ambao ni Mwendesha mashtaka

Mkuu na Mkurugenzi mkuu wa upelelezi wa Taifa la kenya kwa kuhudhuria Sameh Shukry Waziri wa Mambo ya Nje na Abass Kamel Mkurugenzi Mkuu wa upelelezi.

Rais alisisitiza juu ya umuhimu unaofanywa na Misri katika kuimarisha Mahusiano ya nchi mbili pamoja na ndugu yake «Kenya « katika nyanja zote ,hasa katika kubadilishana biashara na uwekezaji na nia ya Misri kuongeza uratibu na kushauriana na upande wa Kenya na Rais Uhuru kinyatta binafsi wakati wa Uenyekiti wa Misri wa Umoja wa Afrika hasa katika yale yanayohusisha na vipaumbele vya kufanya kazi ndani ya Umoja sawa kitaasisi, kisiasa au kimaendeleo jambo linalochangia kufikisha ukuaji na utulivu ambao nchi za Afrika zinahitaji.

Mkutano huo ulishuhudia ubadilishanaji wa maoni kuhusu masuala kadhaa ya kikanda yenye maslahi ya pamoja, ikiwamo maendeleo ya hivi karibuni katika Pembe ya Afrika, pamoja na njia za kusaidia juhudi za nchi hizi mbili ili kupambana na ugaidi na itikadi kali kati ya bara la Afrika, hasa kupitia kuimarisha ushirikiano wa kiusalama na kiupelelezi wa pamoja, pamoja na kufanyika njia za uratibu wa kibara ili kupambana na janga hilo la kimataifa chini ya mwavuli wa Umoja wa Afrika .

Monika alisifu mafanikio ya Mkutano wa Afrika huko Addis Ababa, Februari 2019 chini ya uongozi wa Rais Al-Sisi, Akielezea kuwa mafanikio haya yanawakilisha maendeleo ya mchango wa asili wa Misri wenye mizizi katika Umoja wa Afrika, ambao ulikuwa na athari

kubwa zaidi katika nchi za Afrika kwa kuchangia kusukuma gurudumu la maendeleo barani, kulinda amani na usalama na kushughulikia maswala yake mbalimbali kupitia kuiwekea amani ili kuongoza kazi ya pamoja ya Afrika kipindi cha mwaka 2019. Pia alisisitiza uwepo wa njia nyingi za kuiendeleza njia ya mahusiano ya pamoja na kusukuma njia za ushirikiano kati ya nchi mbili katika nyanja mbali mbali za kirasmi na kiraia.

Novemba16 ,2016, Rais Abdel Fattah Al-Sisi alipomkea Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Kenya, William Roto, kwa kuhudhuria Waziri wa Utalii wa Kenya , ambapo Makamu wa Rais wa Kenya aliwasilisha salamu za Rais wa Kenya kwa Rais Al-Sisi na alimpa barua ya Rais Uhuru Kinyatta inayohusiana na kuimarisha mahusiano ya pamoja na kuongezeka kwa uratibu na kushauriana kati ya nchi mbili.

Wakati wa mkutano huo, Makamu wa Rais wa Kenya alielezea kuthamini kwa nchi yake msaada wa kiufundi uliotolewa na Misri katika uwanja wa kuandaa na kuwawezesha wajuzi katika sekta kadhaa, akisisitiza uhusiano wa kina wa misingi ya undugu na ushirikiano kati ya nchi hizo mbili. Akiashiria umuhimu wa kuendelea na shughuli za kuimarisha ushirikiano kati ya nchi za kiafrika katika nyanja mbalimbali, akisifu katika muktadha huu, upokeaji wa Misri wa mwaka jana kwa Mkutano wa Mikusanyiko mitatu ya uchumi ya Afrika na nia yake ya kuendeleza ushirikiano wa kibiashara na kiuchumi wa Afrika wa pamoja.

Kwa upande wake, Rais Al-Sisi alimkaribisha Makamu wa Rais wa Kenya akisisitiza mahusiano imara yanayojumuisha nchi mbili juu ya ngazi zote na alitaka kufikisha salamu zake kwa Rais wa Kenya akiashiria nia ya Misri kuimarisha ushirikiano kwenye nyanja zote na nchi zote za kiafrika kwa ujumla na hasa nchi za bonde la Mto wa Nile, akisisitiza umuhimu wa kufanya kazi kuongeza mawasiliano na ushirikiano kati ya nchi za kiafrika na kushughulikia miradi ya miundo mbinu kwa ajili ya kukidhi maslahi ya pamoja, akisisitiza umuhimu wa kuongeza faida kutokana na makubaliano ya kibiashara yanayojumuisha kati ya Misri na Kenya na kustawisha ubadilishaji wa kibiashara kati ya nchi mbili ambazo zilifika dola milioni 568 kwa mwaka wa 2016 ili kuendana na mahusiano yao mema ya kisiasa yanayozijumuisha.

Rais alisisitiza kuwepo kwa njia kubwa za kuimarisha ushirikiano kati ya nchi hizo mbili katika sekta kadhaa, hasa kilimo na utalii, kutokana na vyanzo muhimu vya nchi mbili katika sekta hizi, akisisitiza maendeleo ya Misri ya kutoa msaada na ujuzi wake wa kiufundi kwa Kenya katika nyanja mbalimbali.

Mkutano huo ulijadili maswala kadhaa yanayohusiana na maendeleo ya mahusiano ya ushirikiano kati ya nchi mbili.pia walizungumzia kuhusu njia za kuimarisha uratibu na kushauriana kati ya Misri na kenya kuhusu maswala kadhaa ya kiafrika, hasa mwendelezo wa mchakato wa maendeleo katika bara hili, kusaidia nchi za Afrika kutekeleza ajenda ya maendeleo ya Afrika kwa mwaka wa 2063.

Novemba 15, 2015 Ujumbe wa Wanachama wa Tume ya Ulinzi na Mahusiano ya Nje katika Bunge la Kenya wakiongozwa na mbunge Andungu Gitengi ulizuru Misri.Rais Abdelfatah Al-Sisi aliupokea ambapo alisifu maendeleo ya mahusiano ya kiuchumi na Kenya kwa kuzingatia kwamba ni mshiriki wa kwanza wa biashara na Misri katika mfumo wa COMESA, akisisitiza umuhimu wa kuendeleza miundo mbinu na vyombo vya usafirishaji vinavyounganisha kati ya nchi mbili kwa kuangalia lile linalo saidia kuimarisha ushirikiano wa kiuchumi na kubadilishana biashara.

Waziri wa Mambo ya Nje Sameh Shukry alisisitiza umuhimu unaotolewa na Misri kwa kuendeleza mahusiano ya pamoja na Kenya katika nyanja mbalimbali, jambo linalofikisha maslahi ya pamoja ya nchi mbili . Maelezo haya yalikuwa wakati ziara yake nchini Kenya Januari 11,2015 iliyoendelea kwa siku tatu ambapo aliongoza ujumbe wa Misri katika mzunguko wa sita wa Tume ya pamoja kati ya nchi mbili .Pia alikutana na Waziri wa Mambo na Biashara ya Nje wa kenya Amina Mohamed Wakijadiliana mahusiano ya kisiasa ,na kiuchumi na umuhimu wa kuyaendeleza hasa katika nyanja za uwekezaji na biashara ili kufikia maslahi ya nchi hizo mbili . Waziri wa Kenya alisisitiza nia ya nchi yake ya kuongeza kuendeleza mahusiano katika nyanja za ushirikiano katika sekta ya usalama na maendeleo ya rasilimali watu.

Na katika uwanja wa mawasiliano na kunufaika na ujuzi wa kimisri na kupata udhamini wa kozi za masomo kwa wakenya .

Pia aliashiria kwa ushirikiano uliopo kati ya nchi mbili katika mfumo wa COMESA, vile vile Waziri Sameh Shukry alisisitiza kuwa Shirika la Misri la Ushirikiano kwa ajili ya maendeleo lina nia ya kutoa msaada wote kwa ndugu wa Kenya katika nyanja za kujenga uwezo ,kupambana na ugaidi na kutoa msaada wa kiufundi katika nyanja ya usalama na mafunzo mbali na kuendeleza mahusiana ya kiuchumi na kibiashara, akiashiria ushiriki wa wafanyabiashara 50 wa kimisri katika ujumbe wa kibiashara unaofuatana na ujumbe wa kimisri na ulifanyika mkutano wa baraza la biashara la Misri na la kenya kwa kuhudhuria wafanyabiashara kutoka nchi mbili.

Novemba 15,2015, Rais wa Al-Sisi alipokea wajumbe wa kamati ya ulinzi na mahusiano ya nje katika Bunge la kenya wakiongozwa na mbunge Andugu Gitingi. Wakati wa mkutano huo, Rais alisifu maendeleo ya mahusiano ya kiuchumi na kenya kwa kuzingatia kwamba ni mshiriki wa kibiashara wa kwanza kwa Misri katika COMESA,akisisitiza umuhimu wa kuendeleza miundo mbinu na vyombo vya usafirishaji kati ya nchi mbili jambo linalochangia kuimarisha ushirikiano wa kiuchumi na kubadilishana biashara.

Ushirikiano katika uwanja wa kupambana na ugaidi

Misri inasisitiza katika vikao vyote vya kimataifa umuhimu wa kupambana na ufadhili wa ugaidi kwa ufanisi na kuzuia vyanzo vya usajili, kubeba silaha, kuunga mkono na kuwakumbatia kisiasa, pamoja na hitajio la kuunga mkono nchi za Kiafrika zinazokabiliana na ugaidi na kuzisaidia katika juhudi zake za kuuondoa, na mshikamano na waathirika waliopotelewa na watu wao na vikosi vya utekelezaji wa sheria na raia. . Na umuhimu wa kupitisha mtazamo kamili wa kukabiliana na ugaidi ambao unajumuisha kukomesha na sababu za ugaidi na itikadi kali, ikiwa ni pamoja na kupitia maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Ushirikiano wa usalama kati ya Misri na Kenya katika mapambano dhidi ya ugaidi na msimamo mkali ni mojawapo ya nyanja muhimu zaidi za ushirikiano kati ya nchi hizo mbili, kwani nchi hizo mbili zinakabiliwa na changamoto kama hizo kwa sababu ya mashambulio ya kigaidi

kwenye maeneo ya kijeshi na ya kiraia kutoka makundi ya kigaidi yenye itikadi kali , mengi katika hayo ni makundi yaliyo vuka mipaka yamechochewa na itikadi kali na kutafsiri vibaya Uislamu, ambapo Kenya inateseka kutokana na mashambulio ya kigaidi yaliyotokea mara kwa mara na vikundi vya watu wenye msimamo mkali.

Wakati wa mazungumzo yao mnamo Februari 2017, Rais Abdul Fattah Al-Sisi na Rais wa Kenya walisisitiza umuhimu wa kuamsha ushirikiano wa usalama kati ya nchi hizo mbili kwa kuzingatia vita vya pamoja vya nchi hizo mbili dhidi ya ugaidi, na changamoto zinazokumbana nazo kutokana na tishio linaloendelea la vikundi vya kigaidi vyenye msimamo mkali, na katika muktadha huu, Rais Al-Sisi alisisitiza juu ya umuhimu wa jukumu linalofanywa na Al-Azhar katika kusambaza mafundisho sahihi ya dini la Kiislamu na kupambana na itikadi kali. Rais Al-Sisi pia alikaribisha ombi la Rais wa Kenya kuhusu kuongeza idadi ya maimamu na wahubiri wa Kenya waliopata mafunzo kutoka Al-Azhar Al-Sharif.

- Mnamo tarehe 5/6/2015, ujumbe wa ngazi ya juu wa polisi wa Kenya wakiongozwa na Mshauri wa Waziri wa Mambo ya Ndani wa Kenya kuhusu Mambo ya Mafunzo walitembelea Misri, na ujumbe huo ulipokelewa na (Mohammed Al – Hamzawi) Naibu Msaidizi wa Waziri wa Mambo ya nje wa Nchi za Bonde la Mto wa Nile. Pande hizo mbili zilijadili njia za kukuza ushirikiano kati ya nchi hizo mbili katika kupambana na ugaidi na nyingine ni za nyanja za usalama.

  Mnamo Desemba 2018, Misri ilishiriki katika Mkutano wa ngazi ya juu mjini Nairobi kuhusu Amani na Usalama barani Afrika. Balozi Osama Abdel Khalek, Balozi wa Misri nchini Ethiopia na Mwakilishi wake wa Kudumu wa Umoja wa Afrika, alitoa hotuba ya Misri wakati wa ufunguzi wa mkutano huo pamoja na Waziri wa Mambo ya nje wa Kenya Monica Goma na Kamishna wa Amani na Usalama wa Afrika Ismael Sharqi, na Mkurugenzi Mkuu wa Ofisi ya Umoja wa Mataifa huko Nairobi Hana Tita.

- Wakati wa mkutano wake na Balozi wa Misri huko Nairobi, Balozi Khalid Al-Abyad mnamo Februari 2019, Waziri wa Ulinzi wa Kenya Rachel Omano alionesha nia kubwa ya kuimarisha ushirikiano na Misri katika uwanja wa kupambana na ugaidi kama changamoto kubwa zaidi inayoikabili Kenya, akisifu -katika muktadha huu- hotuba ya Rais Al-Sisi wakati wa hafla ya kuchukua kwake Uenyekiti wa Umija wa Afrika huko Addis Ababa na ishara yake kali kwa hitajio la ushirikiano wa juhudi za kikanda ili kukomesha mizizi ya ugaidi katika bara la Afrika.

- Katika mfumo wa ushirikiano wa pamoja kati ya Misri na Kenya kwa ajili ya kupambana na ugaidi, Balozi Hamdi Loza, Naibu Waziri wa Mambo ya nje wa Mambo ya kiafrika, alisafiri kwenda mji mkuu wa Kenya Nairobi ili kushiriki katika Mkutano wa kiafrika wa kikabda wa ngazi ya juu kuhusu kupambana na ugaidi , uliofanyika jijini Nairobi mnamo 10 na 11 Julai 2019. Ushiriki wake unatoka kwa Uenyekiti wa kimisri wa sasa kwa Baraza la Amani na Usalama la Afrika.

Taarifa za Wizara ya Mambo ya nje ya Misri kuhusu mashambulio ya kigaidi nchini Kenya

Misiri umesisitiza msimamo wake pamoja na Kenya na kulaani vitendo vya kigaidi dhidi yake na umuhimu wa kuimarisha juhudi za kimataifa ili kupambana na ugaidi, ambayo ni changamoto ya pamoja kwa nchi hizo mbili kwa sasa.

Mfano wa nafasi rasmi ya Misri katika mshikamano na Kenya katika kupambana ugaidi ni:

- Mnamo Septemba 22, 2013, Wizara ya Mambo ya nje ya Misri ililaani vikali shambulio la kigaidi katika kituo cha biashara jijini Nairobi na liliwaua watu 59.

- Misri ililaani shambulio la kigaidi lililotokea karibu na mji wa Mandira kaskazini Mashariki mwa Kenya, ambalo liliwauwa raia 36, na Misri imesisitiza katika taarifa iliyotolewa na Wizara ya Mambo ya nje siku ya Jumanne, Desemba 2, 2014, kwamba ugaidi ni tatizo la ulimwengu ambalo linahitaji ushirikiano wa juhudi zote ili kukabiliana nalo, hasa ugaidi unaolenga kupoteza usalama, utulivu na maendeleo kila mahali.

- Mnamo Aprili 2015, msemaji wa Wizara ya Mambo ya nje alieleze kuwa Misri inalaani shambulio la kigaidi lililofanywa na kikundi cha kigaidi cha Al-Shabaab katika Chuo Kikuu cha Garissa cha Kenya, ambacho kiliua wanafunzi 150 na majeruhi kadhaa, akitoa pole kwa familia za waathiriwa, na ikitamani uponaji wa haraka kwa waliojeruhiwa, na msemaji huyo amerudia wito wa Wamisri kwa kuunganisha juhudi za kimataifa ili kupambana na matukio ya kigaidi, ambayo yanalenga kupotea utulivu katika nchi zote za ulimwengu, akisisitiza msimamo wa Serikali na watu wa Misri na mshikamano wake na serikali na watu wa Kenya katika kupambana na ugaidi.

- Mnamo Januari 2019, wanamgambo walishambulia kiwanja cha hoteli cha kifahari katika mji mkuu wa Kenya (Nairobi), na kuwauwa watu 21. Kikosi cha wanamgambo cha Al-Shabab, ambacho kinamakazi nchi Somalia kama makao makuu yake na kinaunga mkono Al-Qaeda kilidai kuhusika katika shambulio hilo, na Misri ililaani shambulio hilo vikali , na ilisisitiza juu ya kuunganisha juhudi za kimataifa ili kupambana na matukio ya kigaidi na kuondoa mizizi yake.

Mnamo tarehe 17 Juni, 2019, katika taarifa iliyotolewa na Wizara ya Mambo ya nje, Misri ililaani shambulio la kigaidi kwenye basi lililokuwa limebeba askari wa Kenya karibu na mipaka ya Somalia na Kenya, ambalo lilisababisha vifo vya askari wapatao 10, ikitoa salamu za rambirambi kwa familia za waathiriwa, ikisisitiza kuunga mkono serekali na watu wa Misri na serekali ya watu wa Kenya katika kupambana na matukio ya kigaidi, na ikakariri upya wito wake kwa jamii

ya kimataifa ili kuongeza juhudi zake kwa ajili ya kupambana na jambo hili, ambalo linalenga kupoteza usalama na utulivu katika sehemu zote za ulimwengu.

Msimamo wa Al-Azhar kuhusu ugaidi nchini Kenya

Pamoja na kuongezeka msimamo itikadi kali; na Kenya ikipitia matukio mbali mbali ya kigaidi na kwa mwelekeo wa nchi hizo mbili, Misri na Kenya zilikukubaliana juu ya umuhimu wa kupambana na ugaidi kupitia kuondoa mizizi ya itikadi kali; jukumu la Al-Azhar linakuja, kama ni mojawapo ya taasisi ya kwanza inayotoa huduma zake kubwa kwa Kenya katika uwanja wa mafundisho ya lugha ya Kiarabu na mafundisho ya Kiislamu ya upole na ukweli wa dini, kupitia kwa wajumbe wake au kupitia taasisi za elimu za Azhar.

- Mnamo Aprili 26, 2018, mji wa Kenya (Malindi) kulifanyika mikutano ya siku ya nne ya ujumbe wa amani uliotolewa na Baraza la wanachuoni wa Kiislamu kwenda Kenya, ambapo ujumbe huo ulishiriki katika kikao cha mazungumzo ya dini kilichoandaliwa na Baraza Kuu la Waislamu wa Kenya, mbele ya Wawakilishi wa dini na jamii za Kenya na mwakilishi wa serekali ya Kenya ili Kufadhili mazungumzo ya dini. Wakati wa kikao hicho, wanachama wa ujumbe huo waliwasilisha taarifa ya utangulizi juu ya Al-Azhar kama taasisi ya kidini na ya kielimu, na kuhusu Baraza la wanachuoni wa Kiislamu kama taasisi ya wasomi wa Kiislamu, na aidha kuhusu mradi wa Msafara wa Amani ambao unaangazia ulimwengu ili kueneza utamaduni wa mazungumzo na kuanzisha misingi ya amani ya ulimwenguni.

- Mnamo Novemba 2, 2018, Kikundi cha Kizazi cha Usalama cha Kenya, kwa kushirikiana na Ujumbe wa wasomi wa Al Azhar nchini Kenya, kiliandaa semina kwa maimamu na wahubiri chini ya anuani : «Wajibu wa maimamu na wahubiri katika kukuza amani ya kijamii».

- Mnamo tarehe 27 Februari 2018, Dk Ahmed Al-Tayeb, Sheikh wa Al-Azhar Al-Sharif, alimpokea Sheikh Yusuf Nazibou, Mwenyekiti wa Baraza Kuu la Waislamu wa Kenya, na alisema kuwa Al-Azhar ipo tayari ili kuongeza juhudi na msaada wake mara mbili kwa Waislamu nchini Kenya kupitia kuongeza idadi ya udhamini wa masomo yanayotolewa kwa wanafunzi Kenya huko Al-Azhar, na kufundisha maimamu wa Kenya kukabiliana na maswala na shida za kisasa.

Na kwa upande wake, Sheikh Nazibou alimshukuru Imamu mkuu kwa yale ambayo Al-Azhar hutoa kwa Waislamu wa Kenya katika uwanja wa elimu misaada, akisisitiza kwamba Al-Azhar ni sauti ya Waislamu na Qibla yao ya kielimu, ambayo imedumisha utulivu wa kijamii barani Afrika kwa miongo kadhaa, na bado ni dhamana ya Kulinda watu wa Kiafrika kutokana na tishio la itikadi kali.

Mnamo Oktoba 24, 2016, Imamu Mkuu Ahmad Al-Tayyeb alipokea ujumbe wa Kenya ulioongozwa na Sheikh Ahmad Badawi, Mwenyekiti wa Baraza Kuu la Waislamu wa Kenya, wakati wa Ziara yake mjini Kairo, na mheshimiwa Imamu Mkuu alisisitiza kwamba Al-Azhar inafanya kazi ili kukabiliana na mawazo na mikondo inayoumiza Uislamu na Waislamu, akisisitiza kwamba Uislamu hauna picha hii ya kikatili kama ilivyotolewa, kwa sababu Mwenyezi Mungu hakushusha dini ila kwa ajili ya kheri na furaha kwa wanadamu.

Sura ya Tatu

Mahusiano ya Kiuchumi na ya Kibiashara

Mahusiano ya kiuchumi na kibiashara pamoja na Kenya yanawakilisha mwelekeo muhimu kuhusu mfumo wa mkakati uliopitishwa na Misri kuelekea kuongeza ushirikiano pamoja na nchi za bara la Afrika, ambapo Misri kwa miongo mingi imeendeleza ushirikiano wa kiuchumi pamoja na Kenya katika kiwango cha pande zote mbili au ndani ya mfumo wa vikundi vya kiuchumi vya kikanda ambavyo viliunganisha nchi hizo mbili pamoja, kwani mahusiano hayo yameshuhudia maendeleo mazuri kwa matokeo ya uanachama wa nchi hizo mbili katika COMESA, pamoja na mwelekeo wa Misri kwa ajili ya kutoa mahitaji yake ya bidhaa kutoka nchi za Afrika, ikiamini umuhimu wa ushirikiano kati ya nchi za bara, jambo lenye faida kwa watu wao.

Mkusanyiko wa COMESA

Kundi la COMESA ni moja wapo ya vikundi vya kikanda vilivyofanikiwa zaidi katika bara la Afrika, ambapo ilianzishwa mwaka 1994 ili kuchukua nafasi ya ile iliyojulikana kama eneo la Biashara la Upendeleo kwa nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika liloanzishwa mwaka 1981.

Mkataba wa COMESA ulianza kama eneo la biashara la upendeleo lililolenga kuanzisha eneo la biashara Huru kati ya nchi wanachama ili kuwa muungano wa forodha na baadaye soko la pamoja, na Misri ilitia saini ili kuingia makubaliano tarehe 29/6/1998, na msamaha wa ushuru wa forodha umetumika kwa usafirishaji kwa nchi wanachama kuanzia tarehe 17/2/1999 kwa msingi wa kanuni ya usawa wa bidhaa zinazoambatana na cheti asili kilichoidhinishwa na mamlaka husika katika kila nchi.

Nchi Tisa za wanachama za COMESA zilisaini tarehe 31/10/2000 juu ya Mkataba wa Uanzishwaji wa eneo la Biashara Huru kati ya

Misri na Kenya, na Rwanda na Burundi zilijiunga nao tarehe 1/1/2004, ambapo nchi hizi zitatoa msamaha kamili kwa ushuru wa forodha kwa uagizaji bidhaa kati yao, kwa sharti kwamba bidhaa hizo lazima zifuatane na cheti asili cha COMESA.

Ubadilishanaji wa kibiashara

Thamani ya ubadilishanaji wa biashara kati ya Misri na Kenya ilitofautiana katika vipindi tofauti, kwani baada ya Misri kupata ongezeko kubwa la uuzaji na usafirishaji wake pamoja na Kenya kuanzia 2007 hadi 2010, thamani hii ilishuka katika miaka iliyofuata 2011 kwa sababu ya hali uliyojitokeza katika uchumi wa Misri, kisha serikali ilitilia umuhimu wa kuongeza ushirikiano pamoja na Kenya tangu mwaka 2015.

Mwaka 2007, ukubwa wa biashara kati ya nchi hizo mbili ulifikia dola milioni 320, na kiwango cha mauzo ya nje ya Misri kwenda nchini Kenya kiliongezeka kwa 48.9% na kilifikia dola milioni 176, na ni kwa mara ya kwanza tangu miaka 20, na bajeti ya biashara kwa ajili ya Misri ilikuwa katika ziada ya dola milioni 34.4.

Mwaka 2008, thamani ya biashara ilifikia dola milioni 378.3, na takwimu za kibiashara zinaonesha kuwa usafirishaji wa Misri kwenda Kenya ulikuwa dola milioni 156.2, wakati bidhaa kutoka Kenya zilikuwa dola milioni 222.1 kwa ziada ya dola milioni 65.9 kwa Kenya, ongezeko hilo ambalo halijatarajiwa katika thamani ya usafirishaji wa Kenya kwenda Misri katika mwaka 2008 lilikuwa matokeo ya kuongezeka kwa kiasi na thamani ya usafirishaji wa chai kwenda Misri, ambayo iliwekwa kama waingizaji wakubwa wa chai ya Kenya.

Mwaka wa 2010 ulishuhudia kuongezeka kwa mauzo ya nje ya kimisri kwenda Kenya, kufuatia kushuka kukubwa kwa kubadilishana biashara ya Misri na Kenya kupitia mwaka wa 2009, na hayo ni katika mfumo wa kushuka kwa thamani ya ubadilishanaji wa biashara kati ya Misri na ya nchi nyingi za ulimwengu kwa sababu ya athari ya uchumi wa Misri kwa shida ya kifedha duniani mwaka 2008, ambapo uagizaji wa bidhaa za kimisri kwenda Kenya uliongezeka kiasi cha dola milioni

232,35 katika mwaka 2010 ikilinganishwa na dola milioni 120 kupitia mwaka wa 2009. Na uingizaji wa kimisri kutoka Kenya pia uliongezeka sana katika mwaka huo huo, ambapo uliongezeka kutoka dola milioni 149.3 mwishoni mwa Desemba 2009 hadi milioni 228.66 mwishoni mwa mwaka wa 2010.

Kiasi cha biashara kati ya Misri na Kenya kilifikia dola milioni 640 kwa mwaka 2018 ikilinganishwa na Dola milioni 553 kupitia mwaka 2017 kwa ongezeko la 15,7%, na uagizaji wa Misri kwa soko la Kenya uliongezeka kwa asilimia 21.7% kufikia dola milioni 353 ikilinganishwa na dola milioni 290 katika mwaka wa 2017.

Uingizaji wa Misri kutoka soko la Kenya ulirekodi ongezeko kidogo katika mwaka wa 2018, kwa jumla ya dola milioni 288 ikilinganishwa na dola milioni 263 katika mwaka wa 2017 kwa ongezeko la 9.5%. Na moja ya vitu muhimu zaidi vya usafirishaji wa Misri ambavyo villishuhudia kuongezeka kwa usafirishaji wake katika soko la Kenya: Sukari, Nepi za watoto (Pambers) Vyombo vya kioo, Vifaa vya usafi, na vibao vinavyotumiwa kwa kuandikia.

Usafirishaji muhimu zaidi wa Misri kwenda Kenya: Sukari na Molasi, bidhaa za chuma, Matairi ya gari na betri, bidhaa za karatasi, kemikali na vifaa vya usafi, nyaya na viunganisho, vifaa vya kubadilisha umeme, dawa, vifaa vya uhandisi, vifaa vya kuzuia umeme, vifaa vya nyumbani, mikeka na mazulia, mafuta ya petroli, nta ya Paraffin, viyoyozi, fanicha, PABX, Plastiki za viwandani na Rangi, kauri, zana za afya, Televisheni, Saruji, sabuni, Mbolea, unga, Chokoleti, Pipi, Juisi na Jamu.

Uingizaji muhimu zaidi wa Misri kutoka Kenya ni: Chai, tumbaku, sisal, kemikali, mafuta, matunda na mboga safi, maua yanayokatwa, maua kavu, baadhi ya vitu vya wino wa kuchapisha.

Na nchi hizo mbili zinafanya juhudi ili kuimarisha na kuongeza thamani ya ubadilishanaji wa kibiashara kati yao, na miongoni mwa juhudi hizo :

Julai 2019, ujumbe wa Wamisri ulishiriki kwenye Maonesho na mkutano wa kazi za mkusanyiko wa COMESA 21 wakati wa wiki ya Biashara ya Kenya ya Tatu katika mji Mkuu wa Kenya Nairobi kutoka

17 hadi 21 Julai 2019 na ilihudhuriwa na Marais wa Kenya, Uganda, Zambia, Mauritius na Makamu wa Rais wa Shelisheli na pia wawakilishi wa nchi Wajumbe 21, pamoja na waoneshaji zaidi ya 200 kutoka eneo hilo, na wajumbe walisisitiza kuungwa mkono kwa uongozi wa kisiasa wa nchi hizo mbili kwa juhudi za kuongeza ushirikiano wa kibiashara na kiuchumi kati ya Misri na Kenya ndani ya mfumo wa COMESA na kuunga mkono jitihada zinazolenga kuunganisha vikundi vitatu vya Afrika COMESA, SADC na Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mei 2015, Wizara ya Biashara na Viwanda ya Misri iliandaa maonesho ya kwanza ya usafirishaji wa Misri kwenda bara la Afrika Egypt export expo » katika mji mkuu Nairobi mbele ya mabalozi kadhaa wa nchi za Kiarabu, Mwenyekiti wa chumba cha Biashara cha Kenya, na Wakili wa Wizara ya Biashara ya Kenya, na Maonesho hayo yalifunguliwa na Balozi wa Misri nchini Kenya Mahmoud Talaat , ambapo alisisitiza umuhimu wa ziara kadhaa za wafanyabiashara Wamisri kwani soko la Kenya lina washindani wengi waliopo tangu zamani, ambapo ziara zinahitaji kurudiwa mara kwa mara ili watumiaji wa Kenya waweze kujua bidhaa za kimisri, na alitoa wito kwa wawekezaji wa Kenya watembelee viwanda vya Misri na maeneo ya uwekezaji, na pia alisisitiza haja ya ushirikiano zaidi ili kuboresha mizani ya kibiashara katika usafirishaji na uagizaji bidhaa kwa faida za nchi hizo mbili, akionesha kwamba anataka kuvutia waingizaji wamisri katika soko la Kenya, akibainisha kuwa shida ya usafirishaji ni shida kubwa zaidi inayokabili usafirishaji wa bidhaa za nje kwenda Kenya.

Kwa upande wake, Kibruti Jetoni, Mwenyekiti wa Shirikisho la Chumba cha Biashara cha Kenya, alisema kwamba Kenya ni mlango wa wafanyabiashara na bidhaa za Misri na zaidi ya nchi zingine sita zina mamia ya mamilioni ya watumiaji. Mahali pa Kwenya kijiografia ni sehemu kuu ya kuingiza biashara na kwa nchi za jirani zisizo na bandari kama Rwanda, Burundi, Sudani Kusini, na Uganda kupitia bandari ya Mombasa, ambayo huzingatiwa ni bandari kubwa zaidi katika Afrika Mashariki, na jukumu hili limekua baada ya kufunguliwa kwa reli nchini Juni 2017.

Na alitoa wito wa umuhimu wa kushughulikia kukosekana usawa wa kibiashara kwa faida ya Misri, akiashiria umuhimu wa waagizaji

wa Misri kuzingatia bidhaa maarufu zaidi za Kenya. Zaidi ya kampuni 52 maalumu za bidhaa za viwandani zinazowakilisha halmashauri (6) za usafirishaji zilishiriki kwenye maonesho hayo, ambayo ni, Baraza la usafirishaji Samani, Baraza la usafirishaji vifumwaji, Baraza la usafirishaji vifaa vya Uhandisi, Baraza la usafirishaji vifaa vya ujenzi, Baraza la usafirishaji Fanicha, Baraza la usafirishaji bidhaa za viwanda vya Kemikali, pamoja na Chumba cha kiwanda cha Nafaka ambacho ni mwakilishi wa Shirikisho la viwanda vya Misri.

Septemba 2011, Kampuni ya Al-Nasr ya kuagiza na kuuza nje ilitangaza kupendezwa na matawi yake katika nchi za Kiafrika, haswa zile zilizo katika nchi za Bonde la Mto Nile, na Kenya ni miongoni mwake. Na imekamilisha wazo la kutumia moja ya mali ya kampuni hiyo katika mji Mkuu Nairobi ili kuibadilisha kuwa kituo cha kibiashara cha kimisri nchini Kenya, kwa ajili ya kuonesha bidhaa zote za Wamisri kwa kampuni zenye sifa za kimataifa, haswa samani za nyumbani, vifaa vya nyumbani na umeme. Kwani kampuni hiyo ina tawi kuu jijini Nairobi, na lingine huko Mombasa ili kufuatilia usafirishaji wa vyombo kwenda na kutoka Misri katika bandari, na kampuni hiyo inafanya kazi vizuri katika usafirishaji na kuagiza na kuuza bidhaa za Kenya kwenda Misri kama vile chai, tumbaku ya Kenya, ambayo ni moja ya malengo ya kimkakati ya Misri ambayo huzingatia bara la Afrika kwa ujumla, na nchi za Bonde la Mto Nile hasa, na bidhaa zinazopelekwa na kampuni ya Misri katika soko la Kenya, ni bidhaa za chakula, mboga kavu, juisi na jamu.

Uwekezaji

Kuna uwekezaji mwingi uliobadilishwa kati ya Misri na Kenya, haswa kutoka upande wa wafanyabiashara wa Misri, ambapo Uwekezaji wa Misri nchini Kenya unashika nafasi ya 24 kati ya nchi zinazowekeza katika soko la Kenya kwa jumla ya uwekezaji wa dola milioni 36.6, kwa kulinganisha na uwekezaji wa Kenya unaoshika nafasi ya 80 katika orodha ya nchi zinazowekeza katika soko la kimisri kwa thamani ya uwekezaji wa dola milioni 7.7 zilizosambazwa kati ya kampuni 22.

na kati ya uwekezaji wa kimisri nchini Kenya, kampuni ya Misri ya Citadel Capital, ambayo, tangu Aprili 2014, inamiliki 85% ya hisa za

Rift Valley Railways, mwendeshaji wa reli ndefu kati ya Mombasa na Kampala.

Juhudi za pamoja zinafanywa ili kuimarisha ushirikiano kati ya Misri na Kenya katika uwanja wa kiviwanda, hasa katika sekta zinazohusiana na kilimo na uzalishaji wa wanyama, na ambayo inajumulisha usindikaji wa nyama, ngozi na juisi. Pamoja na kuchukua fursa ya utaalamu wa viwanda wa Misri katika nyanja za kutoa msaada wa kiufundi na mafunzo kwa sekta ya viwandani vya Kenya, na pia kusoma uwezekano wa ushirikiano kati ya pande mbili katika uwanja wa usajili wa dawa kupitia kuwezesha upande wa Kenya kwa taratibu za usajili na kupunguza gharama.

Kamati ya Pamoja

Baraza la Biashara la Misri na Kenya ni moja wapo ya matunda muhimu ya mkakati wa kusaidia ushirikiano wa kiuchumi kati ya nchi hizo mbili, kwani lilizinduliwa wakati wa kazi za kamati ya pamoja kati ya Misri na Kenya Desemba 2016, kwa lengo la kukuza ubadilishanaji wa biashara na uwekezaji.

Mkutano wa kwanza wa Baraza ulifanyika mbele ya Waziri wa Viwanda wa Kenya, Mwenyekiti wa Baraza la Viwanda la Misri, na wajumbe wote wa Baraza hilo kutoka nchi zote mbili. Vyama hivyo viwili vilikubaliana kuunda vikundi vya wafanyakazi walio na jukumu la kuongeza ubadilishanaji wa biashara katika sekta za uhandisi, petrochemical, kilimo, afya, nishati na chakula. Mwenyekiti wa Baraza Hossam Farid alisisitiza wakati wa mkutano na Waziri wa Viwanda na Biashara wa Kenya na ujumbe uliofuatana kwamba kuna sekta kadhaa ambazo Baraza linalenga kuimarisha uwepo wake katika soko la Kenya katika kipindi kijacho.

Ujumbe wa kimisri uliowakilishwa na Baraza la Biashara la Kenya-Kenya ambalo lina kampuni 55 zinazowakilishwa na wafanyibiashara zaidi ya 60 katika sekta hiyo (Viwanda vya Uhandisi - Vifaa vya ujenzi

Viwanda vya kemikali - Viwanda vya Chakula - Sekta ya Afya - Sekta Mbadala ya Nishati na Mazingira - Nguo), na ushirikiano katika sekta ya Afya, kwa kuwa mkutano ulifanyika pamoja na Waziri wa

Afya wa Kenya na wakakubaliana yafuatayo: Mchango wa Maabara ya uchambuzi wa damu (mchango kutoka Farco Misri), mchango wa vitengo 1,000 vya matibabu ili kutibu watu 300 wenye virusi vya C (mchango kutoka kwa Farco Misri), mchango wa kitengo cha kliniki ya kuhamahama kupitia madaktari wa Misri (kilichotolewa na Farco Egypt), pamoja na kukubaliana juu ya kusimamia hospitali iliyopo kwa kuteua wasimamizi na madaktari wa Misri katika sekta zote za kiafya, wakiomba idhini na usajili wa dawa 30 za kimisri kwa uuzaji katika soko, na kupokea ujumbe wa kielimu katika sekta hiyo kutoka Kenya kwa mafunzo na maendeleo katika hospitali za Misri.

Wajumbe wa Baraza pia walikutana na Waziri wa Nishati wa Kenya na pande hizo mbili zilikubaliana kupeleka barua za dhamira kwa kampuni kadhaa ili kuanzisha vituo vya umeme vya jua, ambapo Kampuni ya Taa ya Misri ilitoa barua ya dhamira ya kuanzisha kituo cha umeme wa jua kwa uwezo wa MW 100 utakao fadhiliwa kikamilifu na Misri na kusambaza uzalishaji wake kwa serikali ya Kenya kulingana na ushuru wa ununuzi nchini.

Na Kampuni ya El Swedy Misri ilitoa barua ya dhamira ya kuanzisha kituo cha umeme wa jua wa MW 30 kitakacho fadhiliwa kikamilifu na upande wa Misri na kusambaza uzalishaji wake kwa serikali ya Kenya kulingana na ushuru wa ununuzi nchini, Kwa kuongezea, Kampuni ya Infiniti ilitoa barua ya dhamira ya kuanzisha kituo cha umeme wa jua wa MW 250, ambacho kitafadhiliwa kikamilifu na Misri na kutoa pato lake kwa serikali ya Kenya kulingana na ushuru wa ununuzi wa nchi hiyo.

Katika nyanja ya kilimo, pande hizo mbili zilikubaliana juu ya ushirikiano wa pamoja katika nyanja ya uwekezaji wa kilimo kwa kuwekeza kimisri katika kilimo cha mahindi, soya, mpunga na mazao mengine kulingana na uwezo wa udongo. Inatarajiwa kwamba ushirikiano huu utachangia kuongeza usafirishaji wa nje wa kimisri kama mitambo, vifaa, mbolea za kimisri, vifaa vya kilimo na pampu za umwagiliaji ikiwa ni pamoja na mifumo yote ya umwagiliaji, na sekta ya binafsi ya kimisri ilitoa udhamini wa kozi kwa wafanyikazi zaidi ya 500 katika nyanja hii nchini Kenya.

Makubaliano yalitiwa saini na kuhudhuria kwa Mawazir wa Viwanda, Kilimo, Makazi, wa Kenya na Baraza la kazi kwa ukamilifu, juu ya kutoa agizo la uingizaji na ununuzi kwa makampuni ya kimisri, kwa gharama iliyofikia dola milioni 10, ambayo ni asilimia 5 ya jumla ya idadi ya usafirishaji wa Misri kwenda Kenya kwa mwaka wa 2016 katika sekta za (Viwanda vya uhandisi- Viwanda vya kikemikali – Vifaa vya ujenzi- vyakula - afya)

Mikutano ya pamoja inafanyika kila baada ya miezi mitatu, ambapo maghala ya bidhaa za kimisri yameanzishwa mjini Mombasa kwenye eneo la mita za mraba 50,000. Pamoja na kuazisha kampuni nchini Kenya kwa rasilimali ya Misri ili kuwa kama njia ya ukuzaji wa bidhaa ya kimisri katika eneo la Afrika Mashariki. Na kuanzisha kiwanda cha kupakia na kuhifadhi chai katika eneo la viwanda mjini Ain El-Sokhna ili kusafirishaji kwenda nchi za Ulaya, Ghuba ya Kiarabu na eneo la Mashariki katikati ya bara la Asia.

Novemba 2016, Dkt. Sahar Nasr, Waziri wa Ushirikiano wa Kimataifa, aliongoza ujumbe wa kimisri unaoshiriki katika Mkutano wa Kiwango cha Juu kwa Ushirikiano wa Kimataifa kwa ajili ya Ushirikiano wa Maendeleo katika mji mkuu wa Kenya Nairobi, na mkutano huo ni kama jukwaa la kipekee kwa Marais wa Nchi, Serikali, Mawaziri, wakuu wa taasisi na viongozi wa kimataifa ili kujadili njia za kuongeza ufanisi wa ushirikiano wa maendeleo wa kimataifa, na kuboresha vipaumbele vya maendeleo kwa njia inayofaa na vipaumbele vya nchi na kuchangia kuhakikisha malengo ya maendeleo endelevu.

Na mkutano huo ulihudhuriwa na wazungumzaji zaidi ya 100 na viongozi wa maendeleo 1,500 ulimwenguni kote, na Waziri Sahar Nasr aliongoza pia kikao kidogo kwa anuani «Kisa cha mafanikio ya maendeleo nchini Misri», ambacho kililenga kuonesha mifano ya mafanikio ya ushirikiano kamili kwa maendeleo endelevu huko Misri ya juu, ambalo eneo hilo ni moja ya maeneo yenye uhitaji mkubwa nchini Misri

Novemba 16, 2016, Waziri Mkuu Muhandisi: Sherif Ismail alimkaribisha Naibu wa Rais wa Jamhuri ya Kenya, William Roto, ambapo walikubaliana juu ya ushirikiano katika nyanja ya mafunzo

katika nyanja za usalama na kilimo. Na pia walijadiliana kuhusu mahusiano ya kibiashara kati ya nchi hizo mbili ambayo yanazidi dola milioni 500, akielezea nia yake ya kuongeza kiwango cha uwekezaji kati ya Misri na Kenya, na akiashiria kwamba Visa imeondolewa kwa wamisri wanaotaka kutembelea Kenya.

Kenya na Misri zilikubaliana kuondoa ushuru wa mara mbili juu ya uingizaji kwa nia ya kuboresha biashara kati ya nchi hizo mbili na hayo ilikuja wakati wa ziara rasmi ya Rais El_Sisi nchini Kenya Februari 2017. Uamuzi huo unamaanisha kuwa bidhaa za nchi hizo mbili zitakuwa chini ya ushuru wa uingizaji tu.

Misri ilishiriki katika mkutano wa kiwango cha juu kwa uchumi endelevu uliofanyika katika mji mkuu wa Kenya Nairobi kuanzia kipindi cha Novemba 26 hadi Novemba 28, 2018, ambapo ujumbe huo uliongozwa na Muhandisi Sherif Ismail, ambaye ni Msaidizi wa Rais wa Jamhuri kwa miradi ya kitaifa na ya kimkakati, na Sherif Ismail alitoa hotuba ya Misri wakati wa kikao cha ufunguzi wa mkutano huo, ambacho kilijumuisha kuashiria changamoto za mazingira zinazokabili Bahari, Mito na Maziwa kutokana na uchafuzi wa viwanda, mabadiliko ya hali ya hewa na kiwango cha juu cha maji. Na katika muktadha huu Muhandisi Sherif Ismail alisisitiza kwamba Misri inafanya bidii ili kukabili changamoto hizo juu ya kiwango cha kitaifa katika mfumo wa «Maono ya Misri 2030» kwa maendeleo endelevu, na juu ya kiwango cha bara la Afrika kupitia Ajenda ya Umoja wa Afrika kwa Maendeleo Endelevu ya mwaka wa 2063, hasa katika mfumo wa uenyekiti wa Misri kwa Umoja wa Afrika kwa mwaka wa 2019.

-Muhandisi Sherif Ismail pia alikutana na maafisa kadhaa wa Kenya pembezoni mwa mkutano huo, walioongozwa na Waziri wa Uchukuzi, Miundombinu, Makazi na Maendeleo ya Miji, ambapo walijadili njia za kukuza ushirikiano katika miradi ya makazi ya kati na miundombinu ya Kenya, kupitia kuunda ushirikiano kati ya sekta mbili za umma na binafsi katika nchi hizo mbili na kampuni za Misri zitanufaika na fursa za uwekezaji zinazopatikana katika soko la Kenya.

Machi 2019, Misri ilishiriki na kushika nafasi bora kabisa katika Maonesho ya Kimataifa ya Kenya kwa viwanda vya kemikali za petrol,

plastiki, upakizi na ufungaji. Sehemu hii inajumuisha makampuni 31 ya Kimisri yanayohusika na nyanja hii. Maofisa wa Kenya walisifu kiwango cha bidhaa za Misri na uwezo wake wa ushindani unaoziwezesha kuingia kwenye soko la Kenya.

Ushiriki wa Misri katika maonesho hayo unakamilisha juhudi za Misri katika kukuza ubadilishanaji wa biashara na Kenya na kufungua njia mbele ya bidhaa za Misri kuingia masoko ya Kenya, ambayo ni lango la kikanda ili kuingia nchi za Afrika Mashariki, na hayo yalikuja katika mfumo wa juhudi za Misri ili kukuza biashara ya ndani na ushirikiano wa kikanda barani Afrika kwa kulingana na malengo ya Uenyekiti wa Misri kwa Umoja wa Afrika.

Maendeleo, mafunzo na misaada

Misri na Kenya zina mahusiano ya kirafiki na ya kushirikiana, Misri iliunga mkono na ilitoa msaada wa aina mbali mbali kwa raia wa Kenya wakati wa vipindi vya shida na wakati wa kukabiliana na majanga ya asili kama ukame na mafuriko. Na pia Misri ilitoa misaada mingi na kozi za mafunzo kupita sanduku la kimisri kwa ushirikiano wa kiufundi na Afrika lililo chini ya Wizara ya Mambo ya Nje ya Misri (kisha Shirika la Misri la Ushirikiano kwa ajili ya maendeleo na kupitia Taasisi za kimisri zinazohusika), pamoja na juhudi zake za kuwapeleka wataalamu wa Misri katika mfumo wa ushirikiano wa kiufundi na Kenya katika nyanja za kilimo, maji, mifugo na uvuvi, afya, mawasiliano, usalama, ujenzi wa uwezo na nyanja zingine.

Vikundi vya makada wa Kenya wanapata kozi za mafunzo nchini Misri. Kozi hizi za mafunzo zinajumuisha nyanja za Kilimo, Haidroliki, Mikakati, Usalama, umwagiliaji, Afya, Uuguzi, Utalii na Hoteli, Diplomasia, Jeshi na Safari za anga za ndani.

Kituo cha Kimataifa cha Kilimo pia kinatoa kozi kadhaa katika nyanja za: uzalishaji wa kuku, mboga, huduma za kilimo, uchambuzi wa mradi, utengenezaji wa pamba, idara ya kupambana na wadudu, usimamizi wa maji na udongo, uzalishaji na afya ya wanyama, na Wizara ya Umeme inatoa udhamini wa kozi 17 kila mwaka kwa Kenya.

Machi 2012, Waziri wa Mawasiliano na habari wa Kenya Samuel Bugisio alitembelea Misri ili kufanya makubaliano kadhaa ya pamoja kati ya nchi hizo mbili katika nyanja kadhaa zinazohusiana na mawasiliano na teknolojia ya habari na makubaliano haya yanaongozwa na kuanzisha mifumo ya mafunzo inayohusiana na kutimiza mahitaji ya serekali ya Kenya kutoka kwa makada wenye ustadi wa kiwango cha juu katika nyanja ya Teknolojia ya habari na mawasiliano.

Ujumbe wa Kenya ulionesha umuhimu wa maono ya baadaye ya Kenya katika nyanja ya mawasiliano na Teknolojia ya habari kufikia mwaka wa 2030 na nia ya nchi hizo mbili katika nyanja za kuboresha miundombinu, na kuweka mawasiliano na Teknolojia ya habari kama kipaumbele katika ngazi ya nchi ili kusaidia kukuza miundombinu. Ujumbe wa Kenya pia umetaka kuhamisha utaalamu wa Misri katika nyanja za kukuza viwanda vya rasilimali katika nchi hizo mbili, na kufanya kazi kwa pamoja juu ya kiwango cha bara ili kuendeleza miundombinu.

Sura ya nne
Ushirikiano kati ya Misri na Kenya kuhusu maji ya Mto wa Nile

Misiri na Kenya zimeunganishwa na mshipa mmoja, nayo ni Mto wa Nile, na historia ndefu ya ushirikiano katika ngazi zote. Misri imefanya bidii tangu zamani ili kuunda mahusiano na nchi za Bonde la Mto wa Nile ikiwa ni pamoja na Kenya na kuwasiliana nazo ili kukubaliana juu ya njia bora zaidi ya kutumia maji ya Mto wa Nile ili kunufaisha nchi zote za Bonde la Mto wa Nile, pamoja na kuhifadhi haki ya kihistoria ya Misri katika maji ya Mto wa Nile.

Ushirikiano kati ya nchi hizo mbili unajumuisha upande wa maji ya Mto wa Nile, ushirikiano katika usimamizi wa rasilimali za maji kwa ujumla, ambapo makubaliano ya uelewano kwa mradi wa maendeleo ya Rasilimali za Maji nchini Kenya yalisainiwa wakati wa ziara ya Waziri wa umwagiliaji wa Kenya nchini Misri Agosti 2016, ili kutekeleza miradi ya maendeleo ambayo ni pamoja na ujenzi wa mabwawa 6 ya kukusanya maji na matangi ya kuhifadhi maji, kuchimba visima vya maji 20, na kutekeleza mradi wa majaribio kwa mifumo ya umwagiliaji wa kisasa katika kilimo, na kujenga uwezo wa timu ya kiufundi ya Kenya nchini Misri na Kenya.

Misri na Kenya zilitia saini makubaliano kadhaa ili kuchimba visima 180 vya maji ya ardhini kwa kunywa katika maeneo kame nchini Kenya kupitia udhamini wa Misri kutoka katika bajeti ya Wizara ya Umwagiliaji, ambayo yalitekelezwa mwanzoni mwa mwaka wa 2003 katika hatua nne, na kukamilishwa mwaka wa 2009.

- Mnamo Julai 28, 2011, ujumbe wa kimisri ulioongozwa na Waziri wa Rasilimali za Maji na Umwagiliaji ulishiriki katika mkutano wa Mawaziri kwa mpango wa Bonde la Nile uliofanyika Mjini Nairobi.

- Mnamo Septemba 2011, Balozi wa Misiri nchini Kenya alisisitiza kwamba mahusiano ya Misri na Kenya yanaendelea, na kwamba Kenya inaelewa mahitaji ya Misri kwa maji. Na maofisa wanajua kwamba Mto wa Nile ni mshipa wa uhai wa maisha ya Misr, na kwamba Kenya inategemea maji ya mvua katika kilimo chake, na mahitaji yake yote kwa maji ni kuhifadhi nishati, na Misri inaelewa maono hayo

Katika mfumo wa mpango wa kimisri wa Kuendeleza nchi za Bonde la Mto wa Nile mnamo Juni 2014, wahandisi wengi wa Kenya walipata kozi za mafunzo katika nyanja za mitambo ya kilimo cha mashamba madogo, na katika muktadha huu pande hizo mbili za Misri na Kenya zilisaini makubaiano ya uelewano.

- Mnamo Machi 2015, Wizara ya Rasilimali za Maji na Umwagiliaji ilitangaza kwamba Misri na Kenya zilikubaliana kuandaa makubaliano ya uelewano ili kukuza ushirikiano katika nyanja ya miradi ya maji, hasa uchimbaji wa visima vya maji ya ardhini, mabwawa ya kukusanya maji ya mvua, pamoja na nyanja ya kujenga uwezo na kufanya kozi za mafunzo. Makubliano hayo yalikuja kwenye mkutano uliofanyika nchini Misri kati ya Waziri wa Rasilimali za Maji na Umwagiliaji, Dkt. Hossam Maghazi na Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi wa Kenya Bwana: Felix koski, ili kujadili uimarishaji wa mahusiano kati ya nchi hizo mbili na uanzishaji wa miradi kadhaa katika nyanja za maji na umwagiliaji, hasa kuchimba visima vya maji ya ardhini.

- Mnamo Februari 2016, Dkt. Hossam Maghazi, Waziri wa Rasilimali za Maji na Umwagiliaji, alitembelea Nairobi, nchini Kenya kwa ziara ya siku mbili na alishiriki katika sherehe ya ukumbusho wa mpango wa Bonde la Mto wa Nile ambao ulipitishwa Februari 1999 na mkutano wake wa kwanza

ulifanyika katika mwaka wa 2017, na sherehe hii hufanyika kila mwaka katika nchi miongoni mwa nchi za Bonde la Mto wa Nile na unalenga kuimarisha ushirikiano wa kikanda kati ya nchi hizi kwa ajili ya kuhakikisha maendeleo endelevu.

- Mnamo Januari 17, 2017, Misri ilitoa udhamini kwa Kenya ili kutekeleza mradi wa usimamizi na uboreshaji wa rasilimali za maji nchini Kenya, unaojumuisha kuchimba visima 20 vya maji ya ardhini, na kujenga mabwawa 6 ya kukusanya maji(hifadhi za maji)

Wakati wa mkutano wa Marais wawili wa Misri na Kenya walijadili kuunga mkono juhudi za maendeleo katika nchi za Bonde la Mto wa Nile, ambapo marais hawa wawili walisisitiza umuhimu wa kuendelea kufanya kazi ili kuhakikisha faida kubwa kwa nchi zote za Bonde la Mto wa Nile, kupitia miradi ya pamoja. Na Rais Abdulfattah Al-Sisi alisisitiza wakati wa mkutano wake na Rais Kenyata «Tutaunga mkono maendeleo ya nchi za Bonde la Mto Nile ili kuboresha matumizi ya Mto huu mkubwa kwa faida ya nchi za Bonde la Mto wa Nile kwa ujumla,»

- Mnamo Julai 13, 2017, Mohamed Abdel Aty, Waziri wa Rasilimali za Maji na Umwagiliaji alitembelea Kenya ili kujadili njia za kuongeza ushirikiano wa nchi hizo mbili na nchi za Bonde la Mto wa Nile na kuzindua mradi wa ushirikiano wa pamoja kati ya nchi hizo mbili katika mfumo wa udhamini wa Misri unaolenga kuhifadhi maji ya kunywa kwa maeneo kame nchini Kenya na hayo yalikuja kama zawadi kutoka kwa wamisri kwenda kwa wakenya.

Mnamo Novemba 2018, Mohamed Abdel Aty, Waziri wa Rasilimali za Maji na Umwagiliaji, alikutana na Mawaziri kadhaa wa serikali ya Kenya, na miongoni mwao Mawaziri wa Maji, Usafi wa Mazingira, Kilimo, Umwagiliaji na Serikali za Mitaa, na hayo yalikuwa pembezoni mwa kuhudhuria kwake shughuli za Mkutano wa Uchumi Endelevu Mjini Nairobi, ambapo alijadili na Waziri wa Maji na Umwagiliaji miradi ya Ushirikiano wa pamoja kati ya nchi hizo mbili.

Sura ya Tano
Mahusiano ya kitamaduni kielimu na kimichezo

*Mahusiano ya kitamadun*i

Misri na Kenya zina mahusiano imara ya kitamaduni, na nchi mbili zina historia ndefu ya kitamaduni inayowapa upekee, hivi karibuni taasisi za kitamaduni za nchi mbili zimeanza kufanya matukio, matamsha na maonesho ya kisanaa yanayochangia kwa kiasi kikubwa kuwaweka karibu wananchi wa nchi mbili Misri na Kenya na kufahamu utamaduni wao kwa ukaribu na makubaliano yaliyo sainiwa kati ya Misri na Kenya katika mfumo wa kuimarisha ushirikiano wa kitamaduni kati ya nchi za bonde la Mto wa Nile katika kuimarisha na kuhamasisha ubadilishanaji wa kiutamaduni na kisanaa kati ya nchi mbili na miongoni mwa matukio ya mawasiliano ya kiutamaduni kati ya nchi mbili :

Wakati wa Tamasha la saba la filamu za bara la Afrika huko Luxor mwezi wa Machi 2018, filamu ndefu iliyorekodiwa na kenya ilioneshwa, filamu hiyo inajulikana kwa jina la «Mwezi Mpya» iliyotolewa na Filippa Ndisi Herman. Matukio ya filamu yaonesha safari ya kisiwa cha « Lamu» na baadhi ya mabadiliko yaliyotokea katika jamii na kukibadilisha kutoka mji ndogo na kuwa Mji mkubwa wenye bandari kubwa**.**

Mkutano wa kairo wa michoro wa kimataifa wa kumi na mbili ulioandaliwa na sekta ya mfuko wa maendeleo ya kitamaduni kwa kushirikiana na jumuiya ya michoro ya Misri katika kipindi cha Machi 1 hadi 21,2019 ulipokea msanii wa michoro wa kenya Kwami Nyongo ambaye alipata tuzo kadhaa za kimataifa katika uwanja huu, na filamu

ya «The Legend of Ngong hills» ilioneshwa, filamu hiyo imetolewa na msanii wa Kenya ikifuatiliwa na semina ya sanaa ya michoro katika bara la Afrika.

Mjumbe wa Mambo ya Nje ya Kenya Kurmuz Maina, alisifu katika Tamsha la Aswan la kimataifa la utamaduni na sanaa amani na utulivu nchini Misri akisisitiza kwamba viwango vya amani katika mji wa Kairo na miji mingine ni kubwa zaidi kuliko miji mikuu mingine, akiongeza kuwa alikuwa anatamani nchi yake ishiriki katika Tamsha la Aswan lililoandaliwa na Mamlaka Kuu ya utamaduni februari 2019, lakini mwito uliotolewa kwa nchi yake ulichelewa kidogo, jambo lililofanya nchi yake kutoshiriki akiashiria kuwa Kenya ina bendi za kitaifa 47 sawa na bendi moja kwa kila jimbo nchini Kenya akielezea matumaini yake matukio ya Tamsha lijalo yatashuhudia uwepo wa mpango uliochapishwa kwa lugha ya kiingereza unaokusanya taarifa kadhaa kuhusu Mji wa Aswan na Misri kwa ujumla na kuhusu maeneo muhimu zaidi ya uwekezaji na utalii ili kuwajulisha watakaoshiriki katika Tamsha hili.

Idara ya Tamasha la Luxor kwa Sinema ya Kiafrika ilitangaza kuwa kenya itakuwa mgeni wa heshima wa Tamsha la tisa mwaka 2020

Mnamo Juni 2019, Mamlaka Kuu ya Utamaduni ilishiriki kwa kazi ya kisanii na bendi ya Suhag ya muziki wa kiarabu katika Tamsha la Nairobi la kitamaduni nchini Kenya kwa kushiriki nchi 23 kutoka pande mbalimbali za dunia ambapo bendi hiyo iliimba nyimbo nzuri sana pamoja na kucheza idadi ya nyimbo kadhaa za muziki.

Machi 2019 Ubalozi wa Misri mjini Nairobi alishiriki katika maadhimisho ya maonesho ya Kenya ya Kitaifa katika kusherehekea siku ya Kimataifa ya Maonesho, ambapo ubalozi ulisisitiza katika hutoba yake katika sherehe juu ***ya*** umuhimu uliotolewa na Misri ili kuimarisha njia ya ushirikiano na uelewano kati ya nchi za Afrika ikiwa ni pamoja na sanaa na fasihi za kila aina.

Ubalozi ulikaribisha ujio wa vikundi vya Tamthilia vya Kenya ili kufanya maonesho yake nchini Misri hasa katika ukumbi mpya wa Opera ambao utafunguliwa katika mji mkuu mpya wa utawala, na ushiriki wa Misri unazingatiwa ni wa pili katika uwanja wa Tamthilia

nchini Kenya baada ya ushiriki wa kikundi cha Tamthilia cha Misri katika Tamsha la Kenya la Kimataifa la Tamthilia Oktoba 2018, katika mfumo wa kuimarisha mawasiliano na utamaduni na ustaarabu kati ya watu wa bara la Afrika kama moja ya vipaumbele vya Urais wa Misri wa Umoja wa Afrika.

Kwa kuzingatia mahusiano mema kati ya nchi mbili, Misri ilitangaza kuongeza ushiriki wake katika matamsha ya kitamaduni za kimataifa zilizoandaliwa na Kenya. na Kenya ilikaribisha nia hii na Waziri wa Utamaduni wa Kenya alielezea nia ya nchi yake kunufaika na uzoefu mkubwa wa Misri katika uwanja wa majumba ya makumbusho.

Kuanzia tarehe 27 Desemba - 2010 hadi Januari 2- 2011, Makamu wa Rais wa Kenya Kalonzo Masyoka alifanya ziara nchini Misri akiongoza ujumbe wa ngazi ya juu wa maofisa wa kenya. Wakati wa ziara hiyo Masyoka alizuru Chuo Kikuu cha Alexandiria kwa kuhudhuria Dokta Hend Hanfy Mkuu wa Chuo Kikuu na Dokta Richad Mobai Mkuu wa Chuo Kikuu cha Moi cha Kenya ili kutia saini Mkataba mpya wa ushirikiano katika uwanja wa kubadilishana Madaktari ,wanafunzi, na kuhudhuria mikutano na kubadilishana semina na utafiti wa kisayansi ili kuchangia katika kujadili nyanja mbalimbali za Kisayansi na kitaaluma.

Mahusiano ya michezo.

Michezo inazingatiwa ni moja ya shughuli muhimu sana za kijamii zinazopelekea kuimarisha mahusiano ya kisiasa, kijamii na kiuchumi kati ya watu wa ulimwengu kwa ujumla na hasa watu wa Afrika kutokana na kuongezeka msingi wake mpana wa mashabiki na uwezo mkubwa wa kushindana na hivi karibuni Misri inatumia njia zote ambazo zinawezesha kushirikiana na watu wa bara la Afrika

Katika muktadha huu, Klabu ya Wadi Digla mnamo Oktoba 2016 ilifungua tawi jipya la klabu hiyo katika mji mkuu wa Kenya Nairobi, ikiwa ni klabu ya kwanza ya Misri yenye matawi katika nchi nyingine, kama mpango kamili uliopangiliwa na shirika la klabu ya Wadi degla kwa ajili ya upanuzi ndani ya Misri na nje. Na inajumuisha ufunguzi wa klabu 20 nchini Kenya ikifuatiwa na Ethiopia, Uganda na Tanzania.

Wizara ya Vijana na Michezo, kwa kushirikiana na Jumuiya ya Nchi za Kiarabu, iliandaa « Meli ya Nile ya Vijana wa Kiarabu na wa Nchi za Bonde la Mto Nile» mnamo Septemba 2018.

Amapo Idadi ya washiriki katika meli hiyo ilifikia vijana wa kiume na wa kike 220 wanaowakilisha nchi 24 za Kiarabu na Kiafrika, ambapo ziara ilipangwa huko Aswan kutembelea Bwawa kuu na Hekalu la Philae katika mfumo wa shughuli na programu za «Kairo, Mji Mkuu wa vijana wa Kiarabu 2018» chini ya kauli mbiu ya «Ndoto moja .. Lengo moja», na washiriki walitoa muhtasari juu ya historia ya kila nchi ,tamaduni zake, mila , desturi na vivutio vyake muhimu na mahusiano yake ambayo yanaunganisha Misri hapo awali na sasa .

Juni 9, 2019, Balozi wa Misri nchini Kenya alikutana na Waziri wa Michezo, Utamaduni na Urithi wa Kenya Amina Mohammed ambapo walijadiliana maandalizi ya Kombe la Mataifa ya Afrika kwa mpira ya miguu ambapo misri itakuwa mwenyeji katika kipindi cha Juni 21na Julai 19 ,2019 ambapo timu ya taifa ya nchi yake ya Kenya ilifuzu kwa mara ya kwanza baada ya muda mrefu. Na Waziri wa Kenya alionesha nia yake ya kuzuru Misri na kuhudhuria michuano ya Afrika, vile vile alionesha nia yake ya kuimarisha ushirikiano wa kimichezo kati ya Misri na Kenya kupitia kubadilishana wanariadha na uzoefu kati ya nchi mbili.